



MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

TAHADHARI

Tahadhari inatolewa kwa umma dhidi ya onyo linalosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, likidai kwamba *“kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa yanayoambatana na joto kali, inashauriwa kuepuka kujaza pomoni petroli kwenye magari yao ili kujihadhari na uwezekano wa mlipuko.”*

EWURA inatoa taarifa kwa umma kulipuuza tangazo hilo, kwa sababu halina uhalisia wa kitaalam na halijatolewa na mamlaka yoyote nchini.

Ifahamike pia kuwa matanki ya mafuta ya vyombo vya usafiri yameundwa kitaalam kwa kuzingatia usalama, kusinyaa na kutanuka kwa hewa inapokuwa kwenye joto kali, hivyo, umma na watumiaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanaaswa kutokuwa na wasiwasi na kupuuza taarifa hiyo.

Imetolewa na:

Ofisi ya Mawasiliano na Uhusiano,

EWURA Makao Makuu

DODOMA.